

MKATABA WA UPANGAJI.

Mkataba huu wa leo tarehe 21st mwezi september 2021

KATI YA

ADMIRE OIL LIMITED wa SLP 7494, Dar-es-salaam (ambaye katika mkataba huu ataitwa "MMILIKI" kwa upande mmoja).

NA

UNITED ENERGY LIMITED wa SLP 7494, Dar-es-salaam (ambaye katika mkataba huu ataitwa "MPANGAJI" kwa upande wa pili).

Kwa vile Mmiliki anamiliki Plot no.2092, block u iliyopo mtaa wa kizuiani Mbagala Wilaya ya temeke Dar – es-salaam. Mmiliki atampangisha mpangaji kwenye chumba kimoja iliyopo ghorofa ya kwanza katika jengo hili kwa ajili ya office na mpangaji anataka kupanga kwa msharti yafuatayo:

HIVYO MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO:

1. Mmiliki kwa hiari yake amekubali kumpangisha mpangaji chumba katika eneo hilo na mpangaji kwa hiari yake amekubali kupanga chumba hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja kwanzia tarehe 01 mwezi 10 mwaka 2021 mpaka tarehe 30 mwezi 09 mwaka 2022.
2. Kodi ya chumba hiyo itakuwa Tshs. 50,000/= (shilling elfu hamsini) kwa mwezi. Mpangaji amelipa Tshs. 600,000/= (shillingi laki sita tu) kwa mwaka.
3. Mpangaji atatumia chumba hiyo kwa ajili ya office na mkataba unaweza kurudiwa kwa makubaliano ya pande zote mbili.

MPANGAJI ANAWAJIBIKA KUFANYA YAFUATAYO:

1. Kulipa kodi kama alivyokubaliana na mmiliki katika mkataba huu.
2. Atalipa gharama za umeme anaotumia na maji kulingana na matumizi yake.
3. Mpangaji haruhusiwi kumpangisha mtu mwingine sehemu ya chumba aliyopanga bila kupata idhini ya maandishi kutoka kwa mmiliki.
4. Baada ya muda wa mkataba kumalizika iwapo mpangaji atataka kuendelea au kutoendelea na upangaji katika sehemu hiyo itabidi atoe taarifa ya miezi mitatu (3) kabla ya muda wa upangaji haujamalizika kwa mmiliki na itawalazimu wakubaliane upya na kwa mapatano kwa mkataba mpya.

5. Kwamba mpangaji atakapomaliza muda atakabidhi sehemu aliyopanga bila kuvunja au kuharibu sehemu yeyote ya chumba hiyo.
6. Mpangaji akitimiza masharti ya mkataba huu atafanya biashara kwenye sehemu aliyopanga bila kubughudhiwa na mmiliki au wakala wake.
7. Mkataba huu utatawaliwa na sheria za Tanzania.

KWA KUTHIBITISHA MAKUBALIANO HAYA WAHUSIKA WAMETIA SAINI MKATABA HUU KAMA IFUATAVYO;

IMETIWA saini hapa Dar-es-salaam na **SAID MIRE ARTAN**

kwa niaba ya **ADMIRE OIL LIMITED** ambayo ninafahamu leo hii

tarehe 21 mwezi 09 mwaka 2021.

Saini 

Wadhifa MANAGING DIRECTOR.



IMETIWA saini hapa Dar-es-salaam na **MOHAMED M.HASSAN**

kwa niaba ya **UNITED ENERGY LIMITED** ambayo ninafahamu leo hii

tarehe 21 mwezi 09 mwaka 2021.

Saini 

Wadhifa M.M.

Mkataba umesainiwa mbele ya;

Jina: DAMIAN VICTUS

Wadhifa: COMMISSIONER

Saini: 

Anuani: 6992 DAR ES

